



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION  
AND LOCAL GOVERNMENT

## KAGERA REGION INVESTMENT GUIDE



2019

# UZINDUZI WA MWONGOZO WA UWEKEZAJI MKOA WA KAGERA

Wiki ya Uwekezaji  
Mkoa wa Kagera

Viwanja vya Gymkhana

14 Agosti 2019



Empowered lives.  
Resilient nations.

Mwongozo wa Uwekezaji  
Mkoa wa Kagera  
umetayarishwa kwa msaada  
wa Shirika la Maendeleo la  
Umoja wa Mataifa (UNDP) na  
Taasisi ya Utafiti wa  
Kiuchumi na Kijamii (ESRF)



# Utangulizi

## Mhe Mgeni Rasmi

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ukoo wake na neema alizotujalia katika kuandaa Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Kagera

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa ESRF, Dr. Tausi Kida na timu ya walioshiriki kuandaa Mwongozo - Prof Haidari Amani, Mama Margreth Nzuki, Bw. John Shilinde na mwenzangu, Bw. Mussa Martine, naomba kutoa Shukrani maalum na za dhati kama ifuatavyo;

- ✓ Kwako Mkuu wa Mkoa wa Kagera,
- ✓ Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera,
- ✓ Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa: (Bukoba, Muleba, Biharamulo, Karagwe, Kyerwa, Missenyi na Ngara),
- ✓ Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri zote,
- ✓ Wataalam wa Mkoa na wa Halmashauri zote,
- ✓ Bw. Isaya Tendega ambaye tumeshirikiana pamoja toka wakati wa kukusanya taarifa, pamoja na wadau wote wa Taasisi binafsi na Mashirika ya Umma,
- ✓ Pia kipekee tunawashukuru UNDP kwa kuitikia wito wa Waziri Mkuu, na kusaidia Mkoa Kuandaa Mwongozo wa Uwekezaji. Itifaki imezingatiwa



# Fursa za Uwekezaji

- ✓ Mhe. Mgeni Rasmi, katika kutimiza lengo la nchi kufikia uchumi wa kati na uchumi wa viwanda, Tanzania imechukua hatua mbalimbali za kimkakati kuhakikisha malengo haya yanafikiwa. Hii inaenda sambamba na kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa lengo la kubainisha fursa zilizopo katika kila mkoa.
- ✓ Zifuatazo ni fursa za uwekezaji Mkoani Kagera ambazo zimepewa kipaumbele na Mkoa pamoja na Halmashauri zake:

## Biashara za Mipakani...1

### 1. Ujenzi wa Masoko ya Kisasa Mipakani



**Missenyi (W):** Wawekezaji wanakaribishwa kujenga soko la kimataifa la mazao ya kilimo kwa ubia – hekta 8.9 zimetengwa Mutukula.

**Kyerwa (W):** Ujenzi wa soko la kimataifa la mazao ya kilimo kwa ubia – hekta 1.295 Murongo.

**Ngara (W):** Soko la kisasa la mazao ya kilimo na bidhaa nyingine – hekta 8 Rusumo.

# Biashara za Mipakani...2

## 2.Ujenzi wa Maghala (*Warehouses*)

**Missenyi (W):** Ujenzi wa ghala la bidhaa za kilimo – hekta 3.5 Mutukula.

**Ngara (W):** Ghala la bidhaa za kilimo – hekta 8.2 Rusumo.

**Biharamulo (W):** Ghala la bidhaa za kilimo – hekta 3.24 Lusahunga.



# Kilimo, Misitu na Nyuki ... 1

## 1.Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagilaji wa Vanila, Mpunga na Mazao Mengine

**Bukoba (W)** - 90 hekta; **Missenyi (W)** - hekta 5,463; **Karagwe (W)** – hekta 570; **Biharamulo (W)** – hekta 1,120; **Muleba (W)** – hekta 1,180; **Ngara (W)** - 1,002; na **Kyerwa (W)** maeneo yapo ya kutosha.



# Kilimo, Misitu na Nyuki ... 2

## 2. Kilimo cha Chai



**Bukoba (W):** Hekta 1,576 zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha Chai

## 3. Kilimo cha Mihogo



**Ngara (W):** Hekta 5,000 zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha mihogo

## 4. Kilimo cha Parachichi



**Bukoba (W):** Hekta 1,000 zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha Parachichi

# Kilimo, Misitu na Nyuki ... 3

## 5. Kutengeneza Mizinga ya Kisasa na Ufugaji ya wa Nyuki

**Biharamulo (W):** Wawekezaji wanakaribishwa kufuga nyuki na **kutengeneza mizinga ya kisasa kwa ajili** ya matumizi yao wenyewe pamoja na kuwauzia wengine. Uhitaji wa asali ni mkubwa ndani na nje ya nchi.



# Ufugaji

## Ranchi na unenepeshaji mifugo



**Biharamulo (W):** Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza katika ranchi na unenepeshaji mifugo. Kuna hekta zaidi ya 9,500 zimetengwa maeneo ya Nyabugombe, Mihongora, and Nyambale kwa ajili ya ranchi



# Uvuvvi

## Ufugaji wa samaki, vifaranga na chakula cha samaki

(TZ tunazalisha karibu tani 337,000 za samaki kwa mwaka avs Mahitaji ni karibu tani 731,000 kwa mwaka.



**Bukoba (W), Karagwe (W), Muleba (W), and Kyerwa (W):** Kuna fursa kubwa ya kuwekeza katika **ufugaji wa samaki kwenye vizimba**; **Ufugaji wa samaki majumbani**; **Kuuza vifaa vya kufugia samaki majumbani** yakiwemo matanki; **kufuga samaki wa mapambo na kutotolesha vifaranga vya samaki**, pamoja na utengenezaji wa chakula cha samaki.



# Viwanda....1

## 1. Vifungashio



Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza **vifungashio** kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya kilimo, nyuki, samaki na bidhaa za viwandani. Hekta 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda hicho zimetengwa eneo la **Kemondo, Bukoba (W)**.



# Viwanda.... 2

## 2.Kuchakata Mihogo

**Ngara (W):** Kiwanda cha kisasa cha kuchakata mihogo – Hekta 5 zimetengwa kwa ajili uwekezaji huo.



# Viwanda.... 3

## 3.Kuchakata Chakula cha Mifugo na Samaki



**Bukoba Manispaa:** Utengenezaji wa chakula cha mifugo hasa ng'ombe na kuku pamoja na samaki. Hekta 2 zimetengwa kata ya Buhembe



# Viwanda....4

## 5.Kuchakata Maharage

**Karagwe (W):** Kiwanda cha kuchakata Maharage. Hekta 5 zimetengwa kwa ajili ya kiwanda hicho



# Viwanda....5

## 6. Kuchakata Asali



**Biharamulo (W):** Kuna fursa ya kuwekeza kwenye ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kufungasha asali. Hekta 20 zimetengwa kwa ajili ya kujenga kiwanda hicho.

## 7. Kuchakata Samaki



**Muleba (W):** Kuna fursa ya kuwekeza kwenye ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kufungasha samaki.

# Viwanda.....6

## 8.Kiwanda cha kuchakata Ndizi kutengeneza Mvinyo

Kuna fursa ya kuwekeza kwenye ujenzi wa kiwanda cha mvinyo katika halmashauri ya **Manispaa ya Bukoba** – hekta 1.18, **Kyerwa (W)** – hekta 7.6, **Karagwe** – hekta, **Muleba (W)** – hekta 0.39, na **Ngara (W)** – hekta 5



# Viwanda....7

## 9.Kuchakata matunda kutengeneza *juice* na bidhaa nyingine



Kuna fursa ya kuwekeza kwenye viwanda vya uchakataji wa matunda ili kutengeneza *juice* na bidhaa nyingine. Mwekezaji atajenga kiwanda hicho ndani ya hekta 21.21 zilizotengwa na **Bukoba (W)** kwa ajili ya viwanda na **Karagwe (W)** ndani ya hekta 200.



# Viwanda....8

## 10. Kiwanda cha Kuchakata Maziwa



## 11. Kiwanda cha Kutengeneza Barafu



**Karagwe (W):** Mwekezaji anakaribishwa kuwekeza katika kuchakata maziwa ili kutengeneza bidhaa mbalimbali zitokanazo na maziwa – hekta 30 eneo la Kihanga

**Bukoba (M):** Mwekezaji anakaribishwa kuwekeza katika kiwanda cha barafu – hekta 1.3 kata ya Kifungwa

**Bukoba (W):** Mwekezaji anakaribishwa kuwekeza katika kiwanda cha barafu – hekta 2 kata ya Kemondo

# Viwanda....9

## 12. Machinjio ya kisasa

**Bukoba (M):** Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza kwenye machinjio ya kisasa – hekta 3.32 Rwamishenye.



# Viwanda....10

## 13. Kuchakata Taka Ngumu



**Bukoba (M):** Mwekezaji anakaribishwa kuwekeza katika kiwanda cha kuchakata taka ngumu eneo la Nyanga – hekta 5.4.

Kiwanda kitakuwa na uhakika wa kupata zaidi ya tani 15,000 za taka ngumu kwa siku.

Unaokoa mazingira na kupunguza magonjwa ya mlipuko.



# **Viwanda.... 11**

## **14. Kiwanda cha kuchakata mchanga kutengeneza vioo**



**Bukoba (W):** Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza kwenye ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza vioo.

Mchanga mweupe unaofaa kwa kutengeneza vioo upo wa kutosha.



# Viwanda.... 12

## 15. Maeneo jumuishi ya viwanda *(Industrial Parks)*

**Muleba (W):** Wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza kwenye ujenzi wa eneo jumuishi la viwanda – *industrial park*.



# **Chuo Maalum cha Ujuzi (skills) pamoja na shule za msingi na sekondari**



## **Elimu**

**Mkoa wa Kagera unawakaribisha wawekezaji kuanzisha chuo kitachotoa ujuzi kadri ya mahitaji ya eneo husika.**

Ujuzi unaohitajika ni pamoja na namna ya kuongeza thamani mazao ya ngozi, kilimo, uvuvi, misitu nk.

Pia kuna fursa ya kuanzisha shule za msingi na sekondari zenyenye hadhi ya kimataifa

# Utalii

**Uwekezaji katika  
Hoteli, nyumba  
za starehe,  
kambi za watalii,  
huduma za  
watalii, nk.**



**Halmashauri zote zimetenga maeno kwa ajili ya ujenzi wa hotel na uwekezaji unaofanana na huo.**

Mkoa una vivutio vingi vya utalii na unazidi kukua hivyo uhitaji wa hotel na huduma nyingine ni mkubwa.



# Miundombinu na Masoko...1

## 1. Maduka Makubwa (*Supermarkets*)

**Muleba (W):** Ujenzi wa maduka makubwa – hekta 0.8 zimetengwa  
**Biharamulo (W):** Ujenzi wa maduka makubwa – hekta 4 zimetengwa



# **Miundombinu na Masoko...2**

## **2. Uendelezaji Viwanja vya Mpira**



**Bukoba (M):** Uendelezajiwa wa uwanja wa Kaitaba – ubia.

**Missenyi (W):** Ujenzi wa kiwanja cha mpira na michezo eneo la Bunazi – 3.2 hekta

**Muleba (W):** Uendelezajiwa wa uwanja wa David Zimbihile

# Miundombinu na Masoko...3

## 3. Uendelezaji Bandari

**Bukoba (W):** Ujenzi wa Kituo cha Makontena eneo la Bandari Kemondo - Rwagati. Hekta 10 zimetengwa



# Miundombinu na Masoko...4

## 4. Ujenzi wa Stendi za kisasa za mabasi

**Bukoba (M):** Ujenzi wa Kituo cha Mabasi eneo la Nyanga. Hekta 8.3 zimetengwa

**Biharamulo (W):** Ujenzi wa Kituo cha Mabasi eneo la Nyakanazi. Hekta 1.2 zimetengwa



# Miundombinu na Masoko...5

## 5. Ujenzi wa Kituo cha Magari makubwa



**Missenyi (W):** Ujenzi wa Kituo cha Magari eneo la Mpakani. Hekta 3.5 zimetengwa eneo la Mutukula (ubia)

**Ngara (W):** Ujenzi wa Kituo cha Magari eneo la Mpakani. Hekta 8 zimetengwa eneo la Benako (ubia)

**Biharamulo (W):** Ujenzi wa Kituo cha Magari eneo la Nyakanazi. Hekta 2 zimetengwa (ubia)

# Kuchimba na kuongeza thamani madini



## Madini

**Kyerwa (W):** Uchimbaji wa wadini ya Bati (*Tin*) na kuongeza thamani madini hayo.

**Biharamulo (W):** Ujenzi wa viwanda vidogo vya kuchakata Dhahabu eneo la Nyakahura. Hekta 5 zimetengwa kwa ajili hiyo



## **Nini Kifanyike baada ya Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Kagera**

- Kutengezeza Mazingira ya Kuvutia Wawekezaji k.m. Kuondoa kero na vikwazo visivyo na tija
- Kuandaa Upembuzi Yakinifu (Feasibility Studies), na Maandiko Biashara (Business Plan)
  - Yawe ni maandiko yanayozivutia benki (Bankable Projects) ili yaweze kupata mitaji
  - Tutumie wataalamu tulionao kwenye mabenki na taasisi zingine za kiuchumi kama ESRF, DoE etc
- Kuzitangaza kwa nguvu fursa tulizonazo (Aggressive Marketing)

# Tafsiri Fupi ya Viwanda na Uwekezaji

Ukubwa	Kidogo sana	Kidogo	Cha Kati	Kikubwa
Idadi ya Wafanyakazi	1-4	5-49	50-99	100 au zaidi
Ukubwa wa Mtaji (kwa Tsh )	Chini ya 5 milioni	Hadi 200 milioni	Hadi 800 milioni	Zaidi ya 800 milioni

# **Hitimisho**

**Mh. Mgeni Rasmi,  
Mabibi na  
Mabwana**

**Hizi fursa zilizotajwa  
kwa kifupi ni fursa  
ambazo ukitaka  
kuwekeza hata leo  
ziko wazi na  
mazingira wezeshi  
yameshaandaliwa**

**Maelezo zaidi kuhusu fursa, sababu  
za kuwekeza Kagera, maelezo ya  
Mkoa kwa ujumla, mazingira  
wezeshi, hatua za kufuata ukitaka  
kuwekeza nk. yapo ndani ya  
Mwongozo.**

Natumaini mtapata au mmeshapata  
nakala ya mwongozo ili mweze kupitia  
vizuri na kuwekeza. Pia Mwongozo  
utakuwa unapatikana kwenye  
mtandao kuanzia leo.

***Asanteni kwa kunisikiliza***

# **WAWEKEZAJI MNAKARIBISHWA KAGERA**

